



Fahamu hatari za kutumia mshauri asiye na kibali

Kila mwaka, mamia ya maelfu ya watu wanachagua kuifanya Kanada kuwa makazi yao. Wengi wa wageni hawa huamua kuajiri mshauri wa kuwasaidia kushughulikia mchakato wa uhamiaji au uraia.

Ukijirini mshauri, lazima awe na kibali cha [College of Immigration and Citizenship Consultants](#). Immigration, Refugees and Citizenship Canada (IRCC) itashughulika tu na wawakilishi wenye kibali cha kutoa ushauri au uwakilishi wa masuala ya uhamiaji kwa malipo. **IRCC haitakubali maombi yanayowasilishwa na washauri wasio na vibali.**

Kuajiri mshauri asiye na kibali inaweza kuwa na madhara makubwa

Kuwa makini na watu wanaojiita washauri wa masuala ya uhamiaji lakini hawana kibali cha College of Immigration and Citizenship Consultants. Washauri wasio na vibali wanaweza kukosa mafunzo au elimu sawa na washauri wenye vibali au wawakilishi wengine wanaolipwa (wanasheria na wathibitishaji wa hati za kisheria).

Washauri wasio na vibali hawawekwi kwenye viwango sawa vya maadili kama iliyyo kwa wanachama wa College. Ndiyo maana kutumia mshauri asiye na kibali inaweza kuleta madhara makubwa, kama vile

- kupoteza fedha zako:
 - ~ kulipia huduma ambayo hukupata
 - ~ kulipia huduma za ulaghai

- maombi yako kukataliwa:
 - ~ mshauri asiye na kibali anakuambia utume maombi kwenye programu ambayo huna ustahiki nayo, kwa hiyo maombi yako yanakataliwa
- kuzuiwa kuingia Kanada:
 - ~ mshauri asiye na kibali anakuambia udanganye au ufiche taarifa fulani kwenye maombi yako, na mwishowe huruhusiwi kuja Kanadakwa miaka 5

Kutumia mshauri asiye na kibali inaweza pia kusababisha

- wizi wa utambulisho
- fedha kuibiwa kwenye akaunti yako ya benki au kadi ya benki
- vitisho vya unyanyasaji
- dhuluma

Kwa taarifa zaidi kuhusu kubaini, kuepuka na kuripoti vitendo vya ulaghai, tembelea [Canada.ca/immigration-fraud](#).

Ili kuhakikisha mwakilishi wako wa masuala ya uhamiaji au uraia ameidhinishwa, angalia [Canada.ca/immigration-representative](#).